JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

## MFUKO WA MAWASILIANO KWA WOTE (UCSAF)

# TAARIFA YA MIRADI YA UCSAF




www.ucsaf.go.tz

Ucsaf-Tanzania ucsaftz UcsafT

## UTANGULIZI

### KUANZISHWA KWA MFUKO WA MAWASILIANO KWA WOTE (UCSAF)

Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) ulianzishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Sheria ya Bunge nambari 11 ya mwaka 2006 Sura ya 422 kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa huduma ya mawasiliano kwa wananchi waishio katika maeneo machache ya mijini na maeneo mengi yaliyo vijijini yasiyo na mvuto wa kibiashara kwa watoa huduma za mawasiliano.

Waziri mwenye dhamana ya mawasiliano nchini alipitisha kanuni za uendeshaji wa Mfuko Aprili 2009 na tarehe 1 Julai 2009 Mfuko ulianza kazi rasmi.

### MALENGO YA UCSAF

Malengo ya UCSAF yaliyoainishwa na sheria ya uanzishwaji wake yamejikita katika maeneo yafuatayo:-

01 Kuhakikisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano katika maeneo ya vijijini na maeneo ya mijini yenye mawasiliano hafifu;

02 Kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi na serikali katika utoaji wa huduma za mawasiliano kwa wote katika maeneo ya vijijini na maeneo ya mijini yenye mawasiliano hafifu;

03 Kusisimua maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika maeneo ya vijijini na maeneo ya mijini yenye mawasiliano hafifu;

04 Kutengeneza mfumo kwa ajili ya upatikanaji wa mitandao ya mawasiliano na huduma rahisi na zenye ufanisi katika uzalishaji na upatikanaji katika soko la kiushindani;

05 Kuhamasisha utoaji wa huduma bora katika viwango nafuu na kuhakikisha kuwa teknolojia ya habari na mawasiliano inapatikana vijijini na sehemu za mijini zenye mawasiliano hafifu kwa bei nafuu;

06 Kuhakikisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano kwa wote kwa kuboresha upatikanaji wa huduma za mawasiliano kupitia ushiriki wa sekta binafsi.

## KAZI ZA UCSAF

Katika kuhakikisha UCSAF inafikia malengo yake kama yalivyoainishwa katika Sheria iliyoanzisha taasisi na kwamba inatekeleza majukumu yake, UCSAF ina kazi zifuatazo:-


- ❖ Kubaini maeneo ya miradi ya mawasiliano ambayo yanaweza kupata ruzuku kutoka UCSAF;
- ❖ Kuweka vigezo vya utambuzi wa maeneo ya vijiji vinavyohitaji na ambavyo haviwezi kupata huduma ya mawasiliano kwa sababu havina mvuto wa kibiashara;
- ❖ Kuanzisha mfumo madhubuti wa usimamizi wa fedha za UCSAF; Kuweka vigezo sahihi vya utoaji wa ruzuku kwa watoa huduma za Mawasiliano kwa ajili ya kupeleka mawasiliano katika maeneo yaliyoainishwa;
- ❖ Kufanya tafiti mbalimbali na kufuatilia maendeleo ya mawasiliano katika maeneo ya vijijini na yale yasiyo na mvuto wa kibiashara;
- ❖ Kuishauri Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kuhusiana na mambo yanayohusu Mawasiliano kwa wote;
- ❖ Kupendekeza njia sahihi za kutoa ruzuku kwa ajili ya kupeleka huduma ya mawasiliano vijijini na katika maeneo yasiyo na mvuto kibiashara;
- ❖ Kusimamia kisheria mikataba ya utekelezaji wa majukumu ya utoaji wa huduma za mawasiliano kwa wote;
- ❖ Kuweka utaratibu mzuri wa kusimamia, kukokotoa na kukusanya tozo za Mawasiliano kwa wote kutoka kwa watoa huduma;

## UTEKELEZAJI WA MIRADI YA UCSAF

### MIRADI YA MAWASILIANO YA SIMU

UCSAF imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi kama yalivyoainishwa katika Sheria iliyoianzisha. Mpaka kufikia Januari 2025, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) imefanikiwa kuingia mikataba na watoa Huduma ya Mawasiliano (Makampuni ya simu) kufikisha huduma ya Mawasiliano katika kata 1,974 zenye vijiji 5,102 kwa kujenga jumla ya minara 2,152, ambapo minara yote hii ikikamilika wananchi 29,193,753 watapata Huduma hiyo ya Mawasiliano ya simu kwa uhakika. Hadi kufikia Januari, 2025, jumla ya kata 1,627 zenye vijiji 4,482 na wakazi takribani 24,640,304 wameshafikishiwa Huduma ya Mawasiliano kwa jumla

ya minara 1,783 iliyojengwa tayari katika kata hizo. Utekelezaji unaendelea katika kata 347 zenye minara 369, vijiji 620 na wakazi 4,839,754. Gharama (Ruzuku) za utekelezaji wa awamu mbalimbali za mradi wa Mawasiliano Vijijini ni takribani TZS Bilioni 326.



Mradi huu wa Mawasiliano hutekelezwa kwa ruzuku ambayo hutolewa kupitia UCSAF ikiwa ni mchango wa Serikali katika ujenzi wa miundombinu ya huduma za mawasiliano kwa ushirikiano na watoa huduma na kwamba gharama zingine zote za kumalizia ujenzi wa miundombinu hiyo pamoja na gharama za uendeshaji wa miundombinu hiyo ni wajibu wa Watoa Huduma hao kwa kila mmoja.

Tangu kuanzishwa kwa UCSAF kumekua na ongezeko kubwa la idadi ya wananchi waliofikiwa na mawasiliano hasa maeneo ya vijijini ambapo mpaka sasa 98% ya idadi ya Watanzania wamefikiwa na mawasiliano ikilinganishwa na 45% mwaka 2006 kabla UCSAF haijaanza kutekeleza wajibu wake wa kisheria.

**1,974** Kata **5,102** Vijiji

**29,193,753** Wananchi

**2,152 Minara**

**Hadi Januari 2025**
**Huduma ya Mawasiliano**

**1,627** Kata **4,482** Vijiji

**24,640,304** Wananchi

**1,783 Minara**

**Utekelezaji unaendelea:**


**347** Kata **620** Vijiji

**4,839,754** Wananchi

**369 Minara**



**TZS BILLIONI 326**






## UTEKELEZAJI WA MRADI WA TANZANIA YA KIDIGITALI (DTP)

### UJENZI WA MINARA 758 KATIKA KATA 713 TANZANIA

Serikali kupitia UCSAF inatekeleza mradi wa ujenzi wa minara 758 katika kata 713 ambapo jumla ya wananchi milioni 8.5 watapata huduma hiyo pindi mradi ukikamilika. Mradi huu ni wa muda wa miaka miwili na gharama ya kutekeleza mradi husika ni TZS 126 Bilioni.

Mpaka kufikia Januari, 2025 jumla ya minara 574 ambayo ni sawa na asilimia 75.73% imekwisha washwa kama ifuatavyo: -

**Airtel, minara 134 imewashwa;**

**Vodacom, minara 161 imewashwa;**

**Honora (Tigo), minara 198 imewashwa;**

**Halotel, minara 33 imewashwa; na**

**TTCL, minara 48 imewashwa.**

**TZS BILLIONI**
**126**

## MRADI WA KUBORESHA UWEZO WA MINARA

Kupitia mradi wa Tanzania ya Kidigitali (DTP), mnamo tarehe 13 Mei 2023, watoa huduma (Makampuni ya simu) waliingia mikataba na Serikali ambapo jumla ya minara 304 ilipangwa kuboreshwa (kuongezewa nguvu). Mpaka kufikia Januari, 2025, minara yote 304 sawa na 100% ya utekelezaji wa uboreshaji wa minara iliyokuwa na teknolojia ya 2G tayari imeshaboreshwa (imeshaongezewa nguvu ya 3G/4G) toka kwa watoa huduma. Lengo la kuboresha minara hii ni kuongeza wigo wa matumizi ya mawasiliano ya intaneti ya kasi kutoka asilimia arobaini na tano (45%) mwaka 2020 hadi asilimia themanini (80%) mwaka 2025. Serikali kupitia UCSAF imetumia kiasi cha TZS Bilioni 5.15 katika kutekeleza mradi huu tunatarajia kutawawezesha wananchi kufikiwa na huduma ya intaneti ya kasi.

## MRADI WA KUFIKISHA MAWASILIANO NDANI YA ZIWA VIKTORIA

Serikali kupitia mradi wa Tanzania ya Kidijitali (DTP) inatekeleza mradi mahususi wa kufikisha huduma ya mawasiliano katika kata Kumi (10) kanda ya Ziwa, baadhi ya maeneo yakiwa ndani ya Ziwa Viktoria na baadhi ya maeneo yakiwa pembezoni mwa Ziwa Viktoria.

Watoa huduma za mawasiliano (Makampuni ya simu) ya Vodacom na Honora (Tigo) wapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa ujenzi wa minara katika maeneo hayo, maeneo yakiwa ni Kisiwa cha Kiregi na Mabibi vilivyopo kata ya Bukanda wilaya ya Ukerewe Mkoa wa Mwanza, Kijiji cha, Ijitu iliyopo kata ya Kiloleli wilaya ya Busega Mkoa wa Mwanza, Kijiji cha Mushozi na mwalo wa Igabilo katika kata ya Kaagya wilaya ya Bukoba Mkoa wa Kagera, Kisiwa cha Makibwa katika kata ya Kerebe wilaya ya Muleba Mkoa wa Kagera, Mwalo wa Ebunge katika kata ya Etaro wilaya ya Musoma Mkoa wa Mara, Kijiji cha Kyanyamsana (Mwalo wa Nyamome) kata ya Baraki wilaya ya Rorya Mkoa wa Mara, Kijiji cha Nyabiwe na Mwalo wa Burere katika kata ya Kirogo wilaya ya Rorya Mkoa wa Mara, Kijiji cha Busanga kata ya Nyamtinga Wilaya ya Rorya Mkoa wa Mara, Kijiji cha Chifunfu katika kisiwa cha Lyakanyasi katika kata ya Chifunfu wilaya ya Sengerema Mkoa wa Mwanza na Kisiwa cha Gana katika kata ya Ilangala wilaya ya Ukerewe Mkoa wa Mwanza. Mpaka Septemba, 2024 Kisiwa cha Lyakanyasi, Kijiji cha Mushozi na mwalo wa Igabilo tayari wameshafikishiwa huduma bora na ya uhakika wa mawasiliano ya simu. UCSAF iltatoa ruzuku kiasi cha TZS Bilioni 1.29 kukamilisha mradi huu.

Sambamba na hilo UCSAF kwa kushirikiana na TTCL pamoja na Shirika la Uwakala wa Meli (TASAC) wanatekeleza mradi wa Kimataifa wa Mawasiliano na Uchukuzi Ziwa Victoria (MLVMCT) katika visiwa vya Soswa, Kunene na Kweru lengo likiwa ni kuimarisha mawasiliano ndani ya Ziwa Victoria kiusalama ikiwa ni pamoja na kurahisisha zoezi la uratibu wa shughuli za Utafutaji na Uokoaji pindi majanga yanapotokea ziwani. Hadi kukamilika kwa mradi, kiasi cha TZS Bilioni 1.63 zitatumika.

## MRADI WA KUFIKISHA MAWASILIANO KATIKA OFISI MPYA ZA WAKURUGENZI WA HALMASHAURI

UCSAF inatekeleza Mradi wa kufikisha huduma za mawasiliano katika Ofisi mpya za Wakurugenzi wa Halmashauri zilizohamia katika maeneo mapya ambayo yalikua na changamoto za huduma ya mawasiliano. Mpaka kufikia Septemba, 2024 UCSAF imeshatekeleza mradi huu kwa ushirikiano na Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL Corporation) kwa kufikisha huduma ya mawasiliano katika Halmashuri zote 10 zilizokuwa zimeainishwa. Ofisi za Halmashauri hizo 10 zilizoainishwa katika mradi huu ni Mbogwe DC, Tanganyika DC, Kakonko DC, Rorya DC, Malinyi DC, Mtwara DC, Msalala DC, Nzega DC, Kilindi DC na Pangani DC. Lengo la mradi huu ni kufikisha huduma za mawasiliano ya simu katika Ofisi za Serikali na Halmashauri kwa ajili ya kurahisisha shughuli za Serikali na utoaji wa huduma. Gharama za utekelezaji wa mradi huu ni kiasi cha TZS Bilioni 3.2.

## MRADI WA KUFIKISHA HUDUMA YA MAWASILIANO YA SIMU ZANZIBAR.

UCSAF imekamilisha utekelezaji wa Mradi wa kufikisha huduma za mawasiliano katika visiwa vya unguja na pemba. Mradi ambao Mkataba wake ulisainiwa tarehe 20 Januari,

2022 na kutekelezwa kwa ushirikiano na kampuni ya ZANTEL ambapo jumla ya shehia 38 zimenufaika na jumla ya minara 42 imejengwa visiwani Unguja na Pemba. Lengo la mradi huu ni kufikisha huduma za mawasiliano ya simu kwa wananchi waliokuwa na changamoto za kupata mawasiliano hayo ili kuwawezesha kuboresha shughuli zao za kijamii na kiuchumi ikiwamo kuwawezesha kufanya miamala ya kifedha yaani fedha mtandao na kibenki. Serikali kupitia UCSAF ilitoa ruzuku kiasi cha TZS Bilioni 6.9 kufanikisha mradi.



## MRADI WA KUBORESHA (UPGRADE) MINARA 127 KUTOKA 2G KWENDA 3G/4G.

UCSAF imekamilisha mradi ya Kuboresha/Kuiongezea nguvu (Upgrade) minara 127 iliyokuwa na uwezo wa kutoa huduma ya mawasiliano kwa kiwango cha teknolojia ya 2G ili itoe huduma ya intaneti kwa kiwango cha teknolojia ya 3G/4G. Kupitia mradi huu, TTCL imeongeza uwezo (upgrade) minara 50, Vodacom minara 20, Airtel minara 37 na MIC minara 20. Aidha mpaka kufikia Septemba, 2024 Watoa huduma husika tayari wameshakalimisha Kuboresha/Kuiongezea nguvu (Upgrade) minara yote 127. Lengo la Mradi ni kuongeza wigo wa matumizi ya mawasiliano ya intaneti ya kasi hususan maeneo ya vijijini ili kufikia lengo kuu la kuongeza matumizi ya intanenti kutoka asilimia arobaini na tano (45%) mwaka 2020 hadi asilimia themanini (80%) mwaka 2025. Serikali kupitia UCSAF imetoa ruzuku kutekeleza mradi huu kiasi cha TZS Bilioni 3.61.

# MIRADI YA TEHAMA

## KUFUNGA MTANDAO WA INTANETI KATIKA MAENEO YA WAZI

UCSAF imefanikiwa kufikisha huduma ya intaneti katika maeneo 6 ya wazi ya umma ikiwemo Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Lungemba (Mafinga), eneo la Nyerere Square (Dodoma), Ndaki ya Habari na Elimu Angavu (CIVE, Chuo Kikuu cha Dodoma), Soko la Tabora (Tabora), Kiembe Samaki (Unguja) na Soko la Buhongwa (Mwanza). Maeneo Mengine 17 katika Viwanja vya maonyesho ya Sabasaba ambayo ni Main Gate, Mizigo Gate, Msomali Gate, Sabasaba Hall, DART Gate, Wasanii Area, Windoek, Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda, Kilimanjaro International Hall, TEHAMA Pavilion, Dom Hall, Food Area, Karume International Hall, KizotaGate (Inside), Kobil Gate na Magereza Gate. Lengo la Mradi huu ni Kuongeza wigo na matumizi ya mawasiliano ya kasi (broadband) kutoka asilimia 45 mwaka 2020 hadi asilimia 80 mwaka 2025. Serikali kupitia UCSAF imetumia kiasi cha TZS Milioni 374 ili kufanikisha utekelezaji wa mradi huu.

## UJENZI WA KITUO CHA TEHEMA KILICHOPO BWEFUM-ZANZIBAR

Katika kipindi cha miaka mitatu ya serikali ya Awamu ya Sita, UCSAF imekamilisha ujenzi wa kituo cha TEHAMA katika eneo la Fumba, Mkoa wa Mjini Magharibi Wilaya ya Mjini, ambapo ujenzi wa kituo ulikamilika na kuzinduliwa tarehe 26 Oktoba, 2022 na Mhe. Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kukamilika kwa kituo hiki, kumefanya Wilaya zote 11 kwa upande wa Pemba na Unguja kuwa na vituo vya TEHAMA.

Lengo la Mradi huu ni kuwawezesha wananchi kupata huduma mbalimbali kama kudurufu nyaraka mbalimbali, kupiga simu, kutoa huduma za kutuma na kupokea fedha pamoja na kutumika kama kituo cha mafunzo. Vilevile kituo hiki kinasaidia kutoa mafunzo ya TEHAMA, pamoja na kutoa huduma za intaneti kwa wananchi. Gharama zilizotumika katika utekelezaji wa mradi huu mpaka kukamilika ni TZS Milioni 100.

## UANZISHWAJI WA KITUO CHA MIITO YA DHARURA (CALL CENTRE ZANZIBAR)

Serikali kupitia UCSAF imekamilisha uanzishwaji wa kituo cha Mawasiliano cha dharura (Emergency Call Centre) Zanzibar ambapo jengo la kituo cha TEHAMA cha Kiembe Samaki ambalo ni miongoni mwa vituo 6 vya TEHAMA vilivyojengwa Unguja na kufadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia UCSAF kimetumika. Kituo kimekamilika na kimekabidhiwa kwa Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi tarehe 7 Machi 2022. Lengo la Mradi huu ni kuiwezesha Zanzibar kuwa na kituo kwa ajili ya kuratibu taarifa za matukio ya dharura yanayohitaji uratibu wa pamoja, kwa mfano janga la Moto, Magonjwa ya mlipuko, mafuriko na taarifa zingine zinazoweza kujitokeza. Serikali kupitia UCSAF imetekeleza Mradi huu kwa kiasi cha TZS Milioni 250.8

## MAFUNZO YA TEHAMA KWA WALIMU WA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI

Tangu kuanzishwa kwa Mradi wa Mafunzo ya TEHAMA kwa walimu hadi Desemba 2024, UCSAF imeweza kugharamia na kutoa mafunzo kwa walimu 3,798 toka katika shule 1791 za sekondari na msingi za Serikali Tanzania Bara na Zanzibar, mafunzo ambayo yamekua yakifanyika kila mwaka kuanzia mwaka 2016/2017. Lengo la Mradi huu ni kuwajengea Walimu uwezo wa kutatua matatizo madogo madogo ya vifaa vya TEHAMA vilivyopo mashuleni mwao, ambavyo vimetolewa na UCSAF pamoja ama wadau wengine. Mafunzo haya yamekuwa yakifanyika kwa ushirikiano na Taasisi za elimu ya juu (Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) kwa upande wa Kanda ya Kati, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) kwa upande wa Nyanda za Juu Kusini na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es salaam (DIT) Kwa upande wa Kanda ya Mashariki/ Pwani)

## KUPELEKA VIFAA VYA TEHAMA KATIKA SHULE ZA UMMA

UCSAF imefanikiwa kufikisha vifaa vya TEHAMA katika shule 1,121 ambapo UCSAF imekua ikipeleka vifaa hivyo kwa mgawanyo wa Kompyuta 5, Projekta 1 na Printer 1 kwa kila shule. Lengo la Mradi huu ni kuhamasisha na kukuza uelewa zaidi katika masuala ya TEHAMA kwa wanafunzi katika shule za sekondari na hatimaye kuwarahisishia zaidi mara wafikapo katika ngazi za vyuo vikuu kuwa na uelewa katika masuala

yote yanayohusu TEHAMA. Pia mradi huu unawasaidia na kuwawezesha walimu na wanafunzi kupata nyenzo za kujifunzia na kuwasaidia walimu katika ufundishaji wao. Mpaka kufikia mwezi Desemba, 2024 Serikali kupitia UCSAF tayari imefikisha vifaa hivyo vyenye jumla ya thamani ya jumla ya kiasi cha TZS Bilion 5.94.

## SIKU YA WASICHANA NA TEHAMA (GIRLS IN ICT DAY)

UCSAF imefanikiwa kuwajengea uwezo wanafunzi 1,202 wa kike wa shule za sekondari za umma ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya siku Kimataifa ya msichana na TEHAMA (International Girls in ICT Day). Maadhimisho haya hufanyika Mwezi wa Aprili kila mwaka. Lengo la Mradi huu ni kuhamasisha na kukuza uelewa katika masuala ya TEHAMA kwa wanafunzi wa kike katika shule za sekondari na hatimaye kuchagua fani zinazohusiana na masuala ya TEHAMA. Maadhimisho ni mpango mahususi ulioanzishwa na Shirika la Mawasiliano la Umoja wa Mataifa la Mawasiliano (International Telecommunication Union - ITU).

## MRADI WA KUPELEKA VIFAA MAALUM VYA KUJIFUNZIA KWA SHULE ZENYE WATOTO WENYE MAHITAJI MAALUM

UCSAF imekua ikitekeleza mradi wa kufikisha vifaa vya TEHAMA katika shule zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum ambapo Serikali kupitia UCSAF imepeleka vifaa mbalimbali kulingana na uhitaji katika shule 22. Baadhi ya vifaa vilivyonunuliwa ni pamoja na TV, Braille Machine (Nukta Nundu) Orbit reader (Machine za Kisasa), Laptops, Embosser (Printa ya nukta nundu), Digital voice recorders, Magnifiers. Lengo la Mradi huu ni kusaidia shule zenye watoto wenye mahitaji maalum kwa kupeleka vifaa maalum vya kujifunzia. Hii ikiwa inalenga kuboresha mazingira ya elimu kwa watoto wenye ulemavu au mahitaji maalum, ili waweze kupata elimu bora na kufikia uwezo wao kamili. Kwa kupeleka vifaa maalum vya kujifunzia kwenye shule hizo, kunawapa fursa sawa za kujifunza na kushiriki katika masomo kama wanafunzi wengine. Hii ni hatua muhimu katika kuhakikisha haki ya elimu inatimizwa kwa kila mtoto, bila kujali ulemavu au mahitaji maalum wanayokuwa nayo Mpaka kufikia mwezi Septemba, 2024 Serikali kupitia UCSAF imetumia jumla ya kiasi cha TZS Bilioni 1.8 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

## MRADI WA KUTOA VIFAA VYA TEHAMA KWA AJILI YA KUBORESHA HUDUMA ZA POSTA.

UCSAF inatekeleza mradi huu kwa kushirikiana na shirika la Posta Tanzania. Lengo la mradi huu ni kuboresha utoaji wa huduma za posta kupitia uboreshaji wa miundombinu ya kidijitali. UCSAF imefanikiwa kununua Vifaa vya TEHAMA (PDA) 250 kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma za posta. Vifaa hivi vilikabidhiwa rasmi kwa TPC tarehe 12 Julai 2024. Jumla ya gharama za utekelezaji wa mradi huu ni TZS 161,926,471/-.

## MRADI WA TIBA MTANDAO (TELEMEDICINE)

UCSAF kama mdau wa maendeleo wa ndani umekua ukitekeleza mradi wa Tiba Mtandao (Telemedicine) kwa ajili ya kufadhili ununuzi wa vifaa vya Huduma ya Tiba Mtandao, ukarabati wa vyumba vya na kugharamia huduma za mtandao kwa ajili ya maunganisho ya hospitali.

UCSAF kwa kushirikiana na Kikosi Kazi cha Tiba Mtandao ambacho kiliundwa na watumishi kutoka Wizara ya Afya; Taasisi ya Teknolojia ya Dar es salaam (DIT); Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL); Hospital ya Taifa ya Muhimbili; Taasisi ya Mifupa (MOI); na OR-TAMISEMI wamefanikisha utekelezaji wa mradi huu na hatimaye kuanzishwa na kuzinduliwa kwa huduma ya Tiba mtandao kati ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro na Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili (MOI) ambapo uzinduzi wake ulifanyika tarehe 18 Juni, 2020. Baada ya hapo utekelezaji umeendelea katika hospitali zilizosalia, hospitali hizo ni Hospitali za Halmashauri ya Nzega TC na Chato, vilevile hospitali za Rufaa za Tanga, Ruvuma na Katavi.

UCSAF kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto – Zanzibar imetekeleza mradi wa Tiba mtandao kwa kuiunganisha hospitali ya Mnazi Mmoja iliyopo Unguja na Hospitali ya Abdalla Mzee iliyopo Pemba katika mradi wa tiba mtandao (Telemedicine).

Utekelezaji wa Mradi huu Tiba mtandao una lengo la kuziunganisha Hospitali hizo na hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Taasisi ya Mifupa ya MOI, Taasisi ya Moyo (JKCI) ili ziweze kunufaika na utabibu wa kibingwa unaotolewa katika ya Taifa ya Hospitali ya Muhimbili na MOI. Mpaka kufikia mwezi Juni 2024 Serikali kupitia UCSAF imetumia jumla ya kiasi cha TZS 1.59 Bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi huu.

## MIRADI YA HUDUMA ZA UTANGAZAJI

### KUKAMILISHA UJENZI WA TBC STUDIO DODOMA

UCSAF imekamilisha uboreshwaji wa Studio ya TBC Redio Dodoma ambapo ukarabati wa jengo, ufungwaji wa mifumo ya umeme pamoja na kufunga vifaa vya studio umekamilika na kituo kimekabidhiwa kwa TBC kwa ajili ya matumizi ambapo kituo hiki kinatoa huduma kwa wananchi. Lengo la Mradi huu ni kuboresha usikivu wa radio katika Kanda ya Kati ambayo inajumuisha Mkoa wa Dodoma (Makao Makuu ya Nchi). Maeneo yanayopata usikivu kufuatia kukamilika kwa mradi huu ni Dodoma Mjini, Bahi, Mbande, Kibakwe, Matangisi, Nkulabi, Mloda, Kasera, Mchito na Kinyambwa. Pia baadhi ya maeneo ya mikoa ya Singida, Manyara. Serikali kupitia UCSAF imegharamia kiasi cha TZS Bilioni 1.01 kuiboresha studio hii ya kisasa.

### UJENZI WA MRADI WA TBC KISAKI

UCSAF imekamilisha ujenzi wa mradi wa kujenga kituo cha kurushia matangazo ya Redio ya TBC katika eneo la Kisaki lililopo katika Mkoa wa Morogoro. Ujenzi wa Jengo la Kituo umekwisha kamilika pamoja na kufunga Generator na kujenga mnara. Vifaa vya Redio na "Transmission" vilinunuliwa na kufungwa Kisaki na mtambo ulianza kufanya kazi tarehe 28 Mei, 2021. Lengo la Mradi huu ni kuboresha usikivu wa Redio ya Taifa (TBC) katika eneo la Mradi wa kimkakati wa bwawa la kufua umeme la Mwalimu JULIUS NYERERE (JNHPP) pamoja na maeneo ya jirani ya Kisaki, Sesenga, Milengwelengwe, Dakawa Chini, Bwakila Chini, Dutumi, Mbwade, Kibembawe, Bwakila Juu, Kilengezi, Ululu, Zongomero, Kilengwe, Mgunda, Maharaka, Mgoda na baadhi ya maeneo ya Rufiji. Katika kutekeleza mradi huu Serikali kupitia UCSAF imeweza kutoa ruzuku ya TZS Milioni 592.

## MIRADI YA KUBORESHA USIKIVU WA REDIO JAMII NCHINI

UCSAF kwa kushirikiana na Halmashauri mbalimbali nchini imefanikiwa kujenga na kuboresha studio za Redio Jamii ikiwa ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya Arusha, Halmashauri ya Mpimbwe, Halmashauri ya Ruangwa na Halmashauri ya Mtama. Studio hizi zimejengwa na kufungwa vifaa vya kisasa na Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF). Studio za Redio Jamii iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe ilizinduliwa tarehe 25 Februari 2024, Ruangwa FM tarehe 06 Januari 2024 na Mtama FM ambayo pia inafanya kazi kwa sasa ikisubiri uzinduzi. Lengo la Miradi hii ni kuwawezesha wananchi katika maeneo husika kupata taarifa zenye maudhui yanayopatikana kuzunguka maeneo yao. Mpaka kufikia mwezi Juni 2024 Serikali kupitia UCSAF imetumia kiasi cha TZS Bilioni 2.253 katika utekelezaji wake.

## MIRADI YA KUBORESHA USIKIVU WA REDIO YA TAIFA TBC NCHINI

UCSAF inashirikiana na TBC kuboresha usikivu wa matangazo ya redio na kuhakikisha taarifa muhimu zinawafikia wananchi kwa wakati na kwa ubora unaohitajika. Lengo la Mradi huu ni kuongeza ufikiaji wa taarifa kwa wananchi, kuboresha usikivu wa huduma za mawasiliano ya habari, na kuimarisha maendeleo ya mawasiliano ya umma nchini. UCSAF imefanikiwa kujenga/kuboresha jumla ya vituo 19 kwa ruzuku ya TZS 6,273,974,625.














**MFUKO WA MAWASILIANO KWA WOTE (UCSAF),**
Barua pepe: ceo@ucsaf.go.tz • Simu: +255 26 2965771
Namba ya Bure 0800 110 700 • S.L.P. 1957,
10 Barabara ya UCSAF,
41107 Makulu, Dodoma.

**KANDA YA PWANI**
147 Barabara ya Kajenge • S.L.P 33114
Mikocheni, Dar es Salaam

**KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI**
Jengo la NHIF, Ghorofa ya 7 • 11 Barabara ya Karume,
S.L.P 1850, 53107 Mbeya

**KANDA YA ZIWA**
Jengo la NSSF, Ghorofa ya 6 • Barabara ya Kenyatta
Nyamagana, S.L.P 1800, Mwanza.